



National Arts Council

Tarehe: 14/02/2017

**TANGAZO KWA WASANII NA WADAU WOTE WA SANAA**

**YAH: TAMASHA LA 4 LA KIMATAIFA LA NGOMA NA SANAA ZA ASILI  
LITAKALOFANYIKA KATIKA MJI WA CAIRO NCHINI MISRI KUANZIA  
TAREHE 20-26/04/2017**

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limepokea mwaliko kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo juu ya tamasha la Ngoma na Sanaa za Asili litakalofanyika katika mji wa Cairo, nchini Misri kuanzia tarehe 20-26/04/2017.

Baraza linapenda kuwahimiza wasanii na wadau wote wa sanaa kushiriki tamasha tajwa katika kuonyesha na kutangaza kazi bora za sanaa za kitanzania katika soko la kimataifa. Hata hivyo, washiriki wote wanatakiwa kujigharamia usafiri wa kwenda na kurudi Misri ili kushiriki tamasha hilo. Wenyeji watagharamia usafiri wa ndani na makazi kwa wanakikundi wasiozidi 13.

Maombi kuhusu ushiriki wa tamasha hilo yanatakiwa kutumwa kupitia [drumfestival4@gmail.com](mailto:drumfestival4@gmail.com) kabla ya tarehe 01/03/2017.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali fika Ofisi za BASATA, Ilala, Shariff Shamba, Dar es salaam au piga simu namba. 2863748

Nakutakia maandalizi mema.

**Godfrey L. Mngereza**  
**KATIBU MTENDAJI**

*Barua zote ziandikwe kwa Katibu Mtendaji*

All correspondence to be addressed to The Executive Secretary

BASATA Arts Centre, Ilala Sharif Shamba, P.O. Box. 4779, Dar es Salaam, Tanzania.

Telephone: 2863748/2860485, Fax: 0255 - (022) - 286 0486 E-mail: [info@basata.or.tz](mailto:info@basata.or.tz) Website: [basata.go.tz](http://basata.go.tz)